**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA WAMACU LTD NA.03/2022 KILICHOFANYIKA TAREHE 03/11/2022 KATIKA UKUMBI WA MUSOMA CLUB, MUSOMA MJINI, KUANZIA SAA 15:30PM ALASIRI.**

- **Mahudhurio**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | David Mwita Hechei | - | M/kiti wa Bodi |
| 2. | Samwel Gisiboye Marwa | - | Katibu |
| 3. | Michael Joseph Mugwewa | - | M/M/Kiti |
| 4. | Elius Marwa Samwel | - | Mjumbe |
| 5. | Momanyi Range | - | Mjumbe |
| 6. | Kurwa Nyamhanga Mwita | - | Mjumbe |
| 7. | James Marwa Makorom | - | Mwakilishi |
| 8. | Emmanuel Ndege Bensoni | - | Mjumbe |
| 9. | Julius Makonyo Makara | - | Mjumbe |

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kupitisha kulipa kampuni ya **"MSUMBI ESTATE LTD"** sehemu ya malipo ya uagizaji wa mashine za kuchakata kahawa yenye jumla ya **TZS milioni 307,247,358/=** ambayo ni sawa na 60% ya gharama zote za mashine; na
3. Kufunga kikao.

**AG.Na.01/3: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwaita wajumbe wa Bodi kukutana pamoja baada ya kuwa kikao cha Mrajisi kimeisha majira hayo ya mchana na kuwafahamisha kuwa fedha ya mashine imetoka hivyo ni vizuri kupitia kusanyiko hili la kikao cha Mrajisi wakapitisha sehemu ya gharama kwa ajili ya kumilipa SUPPLIER wa MASHINE ili andelee na taratibu za uagizaji wa mashine. Baada ya kusema hayo alimkaribisha M/kiti wa BODI **Ndg. David Hechei** kufungua kikao.

M/kiti Ndg. David Hechei, alisimama na kufungua kikao mnamo saa tisa **(3:40)** alasiri kwa kuwasalimia wajumbe na kuwataka radhi kwa uchovu walionao ila wamekubali kujadili AGENDA moja muhimu iliyombele yetu. Aidha aliwataka wajumbe kuwa huru katika kutoa

michango yao katika kikao hiki kifupi, baada ya kusema hayo M/kiti alikaa na kumwinua katibu kuendelea soma agenda inayofuata.

**AG.NA.02/3: KUPITISHA KULIPA KAMPUNI YA "MSUMBI ESTATE LTD" SEHEMU YA MALIPO YA UAGIZAJI WA MASHINE ZA KUCHAKATA KAHAWA YENYE JUMLA YA TZS MILIONI 307,247, 358/= AMBAYO NI SAWA NA 60% YA GHARAMA ZOTE ZA MASHINE.**

Katibu alifafanua kuwa amepokea simu ya N**dg Rweyamamu** kutoka Mkao Makuu ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo "TADB" ya kuthibitisha kuwa aidha leo au kufikia jumatatu ya tarehe 07/11/2022 watakuwa wameweka fedha ya mashine pamoja na fedha ya miundombinu. Hivyo ili kuepuka usumbufu pamoja na gharama nyingine ni bora wajumbe mkapitisha ulipaji wa sehemu ya gharama hiyo ili iweze kuidhinishwa na Mrajisi wa Mkoa wa Mara na kulipwa kwa msambazaji(Supplier); kwani kwa mujibu wa Mashriti na Sera ya Uhasibu ya WAMACU LTD, Bodi inaweza kuidhinisha fedha isiyozidi milioni Hamsini tu kwa ajili ya shughuli za chama.

Hata hivyo kwa kuzingatia utaratibu huu wa sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni, zinatoa viwango vya uidhinishaji wa fedha katika Vyama vya Ushirika ambavyo vinazingatiwa katika uandaaji wa miongozo, sera na mashariti ya vyama vikuu na vya msingi. Baada ya melezo hayo, wajumbe kwa umoja wao walikubaliana AGENDA hiyo na kusema kwanza swala hili limechelewa sana kutekelezeka, hivyo kama imewezekana na kuthibitishwa na Benki ni vizuri basi ipitishwe haraka sana kwa ajili ya kutekelezwa.

**AZIMIO.**

1. Wajumbe wameazimia kwa pamoja kupitisha jumla ya **TZS milioni 307,247,358/=** ilipwe kwa kampuni ya **MSUMBI ESTATE LTD** kama malipo ya awali ya uagizaji wa mashine, ambayo ni 60% ya malipo yote.
2. Aidha wajumbe wameazimia kuwa azimio lao lipelekwe kwa Mrajisi wa Mkoa wa Mara kwa ajili ya kuidhinishwa ili Supplier aweze kuwekewa fedha hiyo.

**AG.Na.03/3: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti Ndg. David Hehei, alisimama na kuwashukuru wajumbe wote wa BODI kwanza kwa kukubali kujadili AGENDA hii ya dharura na kutoa michango yao iliyowezesha jambo hili kufanikiwa na hatimaye kwenda kutekelezwa.

Pia aliwapongeza kwa uvumilivu na ushirikiano wao kwani kikao walichokuwa nacho kilikuwa na AGENDA nyingi sana pengine isingewezekana kupata hata dakika moja ya kujadiliwa kwa AGENDA hii ya dharura. Baada ya kusema hayo aliahirisha kikao mnamo saa 10:45 na kuwatakia safari njema wajumbe waendapo majumbani mwao hadi hapo kikao kitakapoitishwa tena.

***Muhtasari huu umesainiwa kwa niaba ya wajumbe BODI na***

| | |
|---|---|
| **.........................................** | **.........................................** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

TAREHE…………………………………..